

**MOMBASA COUNTY ASSEMBLY  
HANSARD REPORT**

Wednesday, 22<sup>nd</sup> March, 2017

The House met at 2:36pm.

*(Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid) in the Chair)*

**PRAYERS**

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Members you may sit down. Yes Clerk?

**MOTION**

**REMOVAL OF STREET FAMILIES, STREET CHILDREN AND BEGGARS  
WITHIN THE COUNTY**

Hon Mohamed Hatimy, yes Hon Saad Faraj.

**Hon. Faraj:** Mr. Speaker, on behalf of Hon Hatimy I would like to take this opportunity to move the Motion on his behalf.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes you can go ahead.

**Hon. Faraj:** Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker sir, I beg to move the following Motion;

*(Hon Faraj moved the Motion)*

THAT AWARE that the County Government is charged with the responsibility of controlling air pollution and other public nuisance under the Fourth Schedule Part 2 (3) of the constitution of Kenya 2010;

FURTHER AWARE that street families, street children and beggars who mostly emanate from the neighbouring Counties are now becoming a nuisance to shoppers, tourists, and locals in commercial and residential areas by begging for food and money;

NOTING THAT the street families, street children, and beggars are mostly children who are between the ages of 10 to 16 years and in most instances, are school drop outs;

FURTHER NOTING THAT the presence of these street families, street children and beggars within the County contravenes some of the local and international laws such as the Children Act, Laws of Kenya, Chapter 141, African Charter on the Rights and Welfare of the Child and UNHCR Convention on the Rights of the Child;

CONCERNED THAT despite valiant efforts by the County government to address the issue of street families, street children and beggars within the County the problem keeps recurring;

I therefore urge the County Assembly to **RESOLVE** that:

1. All street families, street children and beggars be removed from the streets and relocated to appropriate places.
2. The County government works in tandem with other stakeholders that are either government or nongovernmental organizations in addressing this issue.
3. The County government to coordinate its measures in addressing the issue of street families, street children and beggars with neighbouring Counties.

I beg to move this Motion and call upon Hon Kasangamba to second. Thank you.

**Hon. Kasangamba:** Thank you Mr. Speaker, I second the Motion.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Members I now propose the question removal of street families, street children and beggars within the County, yes Hon Saad Faraj, Continue.

**Hon. Faraj:** Naam ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa fursa hii. Mheshimiwa Spika Mswada ambao kwamba umependekezwa katika Bunge hili ni mswada ambao ni wa kusaidia na ni mswada ambao kwamba unapendekeza kwenda kumuondoa kijana huyu kule barabarani na kumpatia mahali ambako kwamba ataweza kuishi katika hali njema.

Ukitathmini na ukiangalia kwa ukaribu hawa ambao kwamba wako barabarani wanaoomba ni wale wako katika hizi barabara ni watoto wetu na ni watoto ambao kwamba wengi wao wanatoka katika Kaunti jirani na ni wajibu wetu sisi ikiwa kweli tuko hapa katika misingi ya kutetea na kuleta maadili mema katika maisha yetu na maisha ya watoto wetu basi ni wajibu wetu tuweze kusimama kidete kuangalia njia gani mwanzo wale watoto wale tutawaregeshe mashuleni; tutaweza kuwajua vipi familia zao, ziko sehemu gani na pia kuangalia kuwa wameweza kupata mapenzi yale ambayo kwamba inafaa kwa mtoto na familia yake.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika katika ile hali ya kutathmini haya yote ni wajibu wetu kuangalia kwa ukaribu namna gani sisi kama wanadamu na sisi kama viongozi katika Kaunti hii ya Mombasa tutaweza kuwasaidia watu kama hawa na watoto wetu hawa ili kuwabadilisha maisha yao yawe ni maisha ambayo kwamba ni mema na mazuri ili waishi kama vile wanavyoishi watoto wetu majumbani mwetu.

Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Caroline.

**Hon. (Ms) Auma:** Mheshimiwa Spika Mswada huu ni mzuri lakini tunapenda kurudia mambo ambayo kila wakati tunayatengeneza.

Mheshimiwa Spika mswada huu kuna wakati uliletwa katika Bunge hii na kuwa inatengenezewa sheria kamili kwa sababu hili ni ombi tu tunaomba na kulikuwa kuna sheria inaenda kutengenezewa ili kuje sheria ambayo yaweza kufuatwa katika Kaunti nzima.

Mheshimiwa Spika miezi sita ikipita Mswada unaweza kurudishwa lakini kama umetengenezewa sheria.....

*(Interruption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes what is it Hon Mary Akinyi.

**Hon. (Ms) Akinyi:** Thank you Mr. Speaker I would like to inform this House that we have a Bill which was passed in this House on Childs care and even bringing this Motion in this House is just to give the Bill which was brought here some points to make it heavy so that it can be worked out and this thing although it was brought here in this House but six months are already over that's what i had wanted to inform the House and get informed. Thank you.

**Hon. (Ms) Auma:** Mr. Speaker I know very well the Bill was brought in the House, and the thing which needs to be done in this House, the amendment of the Bill should be done, there is no need of coming back with a Motion and telling us you are enforcing the Motion so that it can be worked on Mr. Speaker.....

*(Interruption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Caroline are you supporting the Motion or you are opposing the Motion?

**Hon. (Ms) Auma:** Mr. Speaker let me emphasize what am saying and then I'll let you know if am supporting or opposing the Motion at the end of my point.

Mr. Speaker this is an Assembly, we need to implement things, if you can bring this here and then they are not willing to implement, I think the last year December there was no any child in the street, the County Secretary was walking around and removing children on the street, and if that thing was to be done even now, there would be no any child on the street of Mombasa.

Mr. Speaker I do support the Motion but the implementation must be done. Thank you.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Kasangamba.

**Hon. Kasangamba:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika ni vizuri Mheshimiwa aliyetangulia kuzungumza amesema anaiunga mkono hoja hii.

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika labda tukumbushane tu katika kumbu kumbu za Bunge letu, nikikumbuka Mswada kama huu uliwahi kuletwa mwaka 2013 na Mheshimiwa Marehemu Amina Zuberi Mheshimiwa Spika...

*(Applause)*

Wakati huo nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Watoto na Elimu Mheshimiwa Spika, na baada ya muda tena iliwahi kuletwa Mswada huu, kwa hivyo hata wale waliokuwa wakifanya kazi walikuwa wakifanyia kazi Mswada uliopita.

Mheshimiwa Spika nafikiri kuna mengi yaliyoendelea kupitia huu Mswada ulioletwa; mimi mchango wangu katika suala hili labda tuelezane kiuchache katika hizi familia tunazosema au katika hawa watoto wanaoranda randa katika mitaa.

Mheshimiwa Spika mimi nitatoa mifano miwili tu, ambayo mmoja unanihusu mimi mwenyewe, miaka ya nyuma kabla sijakuwa Mheshimiwa Mwenyezi Mungu aliniruzuku nikaweza kujenga nyumba ya Kiswahili nikawahi kupangisha na ile nyumba yangu ilikuwa haijafika ile kiwango inayotakikana ikabidi tu niamue kuiweka wapangaji rejareja.

Mheshimiwa Spika wale wapangaji wangu wa miaka hiyo, hata sasa hivi ukienda najua mahali pale anapokaa pale Makadara, kwa hivyo walikuwa matajiri wangu wale watu na kunilipa kodi.

Kwa hivyo inamaanisha ile ni kazi watu wanafanya kuomba omba na mtu anapokuwa na watoto wengi basi anakuwa na watu wa kumuokotea pesa nyingi Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kama hawezi kulipa kodi haijamaanisha ni masikini ile ni njia ya kutafuta uchumi, na kwa ushahidi zaidi ilikuwa yafikia muda ikiwa pesa zimechelewa zaidi anasema anasubiri chama.

Mheshimiwa Spika wale hucheza chama *the so called Merry go round* na mtu akipata anarudi kwao nyumbani kwenda kujenga nyumba na kununua mbuzi na kujiendeleza katika miradi mengine.

Mheshimiwa Spika ni suala la kusikitisha sana lakini yote haya lazima tusimame vikali na tuzidi kulikemea hili jambo kwa sababu ni maisha ya hawa watoto ndio yanaathirika, utapata ni mama mtu mzima yuko pale lakini amechukua wajukuu, saa nyingine akipata mtoto yoyote yuajua mtoto kwake ni chumo zaidi.

Kwa hivyo wale watoto hawasomi hawapati fursa ya kusoma, saa nyingine hupata maradhi ya vifua kwa sababu ya kulazwa nje na baridi, wale watu wamepanga nyumba maeneo mengine ya mji lakini huwa wakija huku wanakaa kiasi ya wiki moja basi wakiona ile siku sio nzuri ya kupata pesa basi wanarudi nyumbani kwenda kulala kwa nyumba zao, lakini ni watu waliopanga nyumba na ni watu wa kujiendeleza na ni watu wa kuangaliwa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika sisi kama viongozi hatuwezi kaa tukaruhusu suala kama hili ttukiangalia yule mtoto ndio nguvu za kesho, za kujenga taifa letu la Kenya, ikiwa tutaelekea hivi inamaanisha baada ya miaka kadhaa tutakosa kukaa katika nchi yetu, katika jimbo letu hili la Mombasa.

Mheshimiwa Spika kwa hivyo mimi kwa kupitia mfano huu nasisitiza huu Mswada uchukuliwe hatua na hatua zake ziwe ni za kudumu, isiwe hatua tu kwa sababu Mswada umetolewa basi baada ya siku mbili yule mtu awe amezembea kwa sababu hawa watu kama Mheshimiwa alivyosema kwamba wakati wa Disemba ilikuweko hakuna hata watoto wa kuomba omba katika mitaa, lakini baada ya muda twawaona askari wakizembea nao familia wanazidi kurudi katika mitaa.

Kwa hivyo mimi ningeomba Mheshimiwa Spika kupitia cheo chako, uamuzi wako uwe mkali wa kuwa watu watakaohusika kutekeleza suala hili, wawe walitekeleza na liwe lenye kuendelea lisiwe mara moja na kuondoka. Ahsante.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Mwadziwe of Mwakirunge.

**Hon. Mwinga:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi labda nitaanza kusema ya kwamba ile Kaunti ambayo ina mambo mazuri lazima ifuatwe na wageni.

Mheshimiwa Spika nasema hivyo kwa sababu Kaunti yetu ya Mombasa imejaaliwa inayo watu ambao wanajiweza na ukiangalia katika hali zao za kidini ni watu ambao kila Ijumaa wanatoa zaka na ndio maana Kaunti yetu inapata wageni wengi sana.

Na Mheshimiwa Spika mswada ulioletwa hapa ni mzuri lakini nimesimama hapa kuupinga...

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika Mswada huu naupinga kwa sababu....

*(Interruption)*

**Hon. Kasangamba:** Point of Order Mr. Speaker.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Kasangamba.

**Hon. Kasangamba:** Mheshimiwa Spika mimi nataka kusema hili ni Bunge la kisheria na iwapo utasema jambo lazima liwe sawa sawa na Katiba yetu, sawa sawa na sheria zote zilizo kuu kuliko sheria zile tunazojua.

Mheshimiwa nafikiri amezungumza kuwa kuna familia zinazokuja mjini Ijumaa kwa sababu ya zaka na tunajua kuwa Ijumaa ni siku ya shule mtoto ameridhi yeye kupitia kwa mchango wake anamaanisha kwamba mtoto asiende shule aje achukue zaka na mamake kwa sababu ni mji wa kidini. Kwa hiyo mchango wake uko kinyume na Katiba yetu Mheshimiwa Spika.

**Hon. Mwinga:** Mheshimiwa Spika mimi nilikuwa nataka kusema ya kwamba ninaupinga Mswada huu kwa sababu familia hizi zimeishi, zimefanya makao katika Mombasa Kaunti na mimi mwenyewe nishawahi kushuhudia juzi tu wakati usajili wa upigaji kura ulipokuwa ukiendelea nishawahi shuhudia hawa watu wakichukua kura na wamechukua kura katika Kaunti yetu wa Mombasa.

Hivyo basi endapo tutaenda kuwafukuza watu hao Mheshimiwa Spika na kura zimefika tutakuwa tunapoteza zile kura...

*(Laughter)*

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika naupinga kwa sababu wakati huu si wakati wa kwamba tuweze kuondoa hizi familia...

Mheshimiwa Spika jambo lengine la kusikitisha watu hawa kama vile Mswada ulivyosema tuwatoe tuwatafutie makao tutawatafutia makao mahali gani? Kwa sababu Mheshimiwa Spika hawa watu wamezoea kukaa ndani ya mji kwa sababu wanajua ndani ya mji ndio kuna watu wengi na hawa watu ndio wanaowasaidia.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika tunapowatoa hawa watu tuwafukuze nje ya mji; hakuna mtu atakayewashughulikia tena na hawa ni watu wana familia, kuna wengine wanafundisha watoto kupitia kwa pesa ambazo wanazipata za hisani ya watu.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi naona Mswada huu ni mzuri lakini umepitwa na wakati, tutakapowafukuza watu hawa tunafukuza kura zetu za Mombasa Kaunti.

Kwa hivyo mimi naomba Mswada huu umepitwa na wakati waheshimiwa wenzangu tuungane tuweze kuuangusha ili kura zetu zibakie hapa tusizifukuze. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Patrick Siminyu.

**Hon. Siminyu:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. Mr. Speaker as I stand that there's a budget of this issue that is budgeted by the National government then the County government should work hand in hand so that they can find solution to this matter.

Hon Speaker you will find that our children are passing through difficult times because of the kind of life they are living, and it is up to the County government to look in to the solution on how we can assist these street children.

Mr. Speaker as you understand that there are no jobs nobody will want to be on the streets and the situation actually forces this person to be on the streets so that he can meet his needs, we know that some of them can survive without a meal then I direct this Motion to want to take care of the situation but it has to be handled with care because when we pass a Motion somebody can misinterpret it so that can mistreat the street families.

So as long as you want to remove them we must have a proper planning Mr. Speaker and where are we going to take them and how are we going to handle these street children and what programs are we having for these children.

Mr. Speaker as much as I want to support this Motion, what I want is to caution the House as we pass this to let us make sure that there's a proper arrangement to handle these street families. Thank you Mr. Speaker Sir.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Mary Akinyi.

**Hon. (Ms) Akinyi:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kuunga mjadala huu mkono...

*(Applause)*

Kwa sababu Mheshimiwa Spika mtoto yeyote yuko na sheria zake ama mwanadamu yeyote ambaye anapumua yuko na sheria zake ama kila mtu, mtoto au mwanadamu ambaye anapumua yuko na haki zake, mtoto yuko na haki ya kuelimishwa, haki ya kula, haki na kulelewa vizuri vile inavyohitajika.

Mheshimiwa Spika hata saa hizi ukipata ukiwa unaenda pale Tarbush saa saba mchana utapata kama watoto wamezunguka pale wanaomba chakula na hao watoto wakati ule anaendelea kuomba chakula ni wakati wanahitajika wawe shule ndio kwa sababu unaona hata shule zengine kuna mipango ambayo imewekwa mashuleni kwa sababu ya watoto waweze kupata chakula katika mashule, kuna mipango ya chakula katika mashule.

Ni kwa sababu ya hizi shida ambazo pengine hawa wanapata wakiwa wanaishi kwa mabarabara Mheshimiwa Spika, na hawa watu ambao wanaoishi kwa barabara ni lazima tuwatoe ndio tuweze kujua shida za watu zinaelekea wapi?

Mheshimiwa Spika hata ukipita katika hiyo njia mimi toka sasa ni miaka minne ninapita kwa ile njia lakini mara kwa mara nikiwa napita mwaka huu unapata mama yuko na mtoto nikipita tena mwaka ujao mama ana mtoto mdogo huyu mtoto sio ati hakui kila mara anazaa huku kuzaa kwa huyu mama huwa anapachikwa hizi mimba wapi? Si anapewa nyumbani ama anapewa hapo barabarani ama ni kwa sababu ya raha zake ndio sababu anaendelea kupachikwa hizi mimba ambazo anaendelea kujaza familia hapo katika barabara, kwa sababu kusema kweli kama hauna uwezo wa kuweza kujimudu huwezi kuendelea kama unazaa zaa kila mwaka na hali kuna upangaji wa uzazi.

Mheshimiwa Spika hizi familia ni lazima tuzitoe kwa mabarabara...

*(Interruption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Member from Mwakirunge what is it?

**Hon. Mwinga:** Mheshimiwa Spika naona Mheshimiwa ambaye anaendelea kuongea anajaribu kupotosha Nyumba hii na Mheshimiwa Spika mama akipata mtoto ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu...

*(Applause)*

Haijalishi mtoto atalishwa nini wala nini? Kuna wamama wangapi wanalia wanatamani wapate watoto hawapati, mama kama yuko *fertile* anapata watoto wacha aendeleo kupata watoto. Ahsante.

*(Applause)*

**Hon. (Ms) Akinyi:** Ahsante zaa watoto ambao unaweza kuwaelimisha, watoto ambao wanaweza kula, watoto ambao wanaweza kuwa na afya inayohitajika, si kuzaa zaa tu kama



ambaye umewekwa majira ya kuzaa, kuzaa inatakikana unazaa watoto ambao unaweza kuwapatia haki zao zile zote ambazo wanahitaji.

Ndiposa Mheshimiwa Spika tukiwa tumetoka hizi *street families* katika mabarabara ndio tutaweza kujua zaidi shida ambazo wanazopata; kuna msembo ambao unasema kuwa ukitaka kujua mwenye mbwa mpige mbwa mwenyewe atafanya nini atajitokeza, tukiwakamata hawa watoto wenyewe watajitokeza.

Unaona hata hivi punde kuna jamaa ambaye yuko katika barabara ambaye aliokota laki mbili na akamrudishia mwenyewe na ilipatikana kumbe yule ambaye alipata laki mbili hata karudishia mwenyewe ni mtu ambaye yuko na kisomo amesoma mpaka chuo kikuu na baada ya huyu kupata zile pesa ndio watu wakaelewa kumbe kuna mtu ambaye yuko na kisomo na kuna vitu vilifanya aende barabarani aweze kusaidika.

Kwa hivyo tukianza huu msururu wa kutoka watu, hizi familia katika barabara tutapata watu ambao ni wazuri kabisa ambao wataweza hata kuendeleza hii Kaunti yetu ya Mombasa na pia katika ile *Bill* ya *childcare* kuna kipengele ambacho kiko pale kwa *Bill* ambao kuwa serikali ya Kaunti inajenga *rescue centre* na hawa watoto tukiwa tunawapata tutakuwa tunawachambua kama karanga wale ambao watakuwa hawana mahali kabisa tutawapeleka katika *rescue centre* na wataendelea na maisha yao vile inavyohitajika. Ahsante.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon Zainab Said Ali.

**Hon. (Ms) Zainab Said:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa hii nafasi mimi naunga mkono kabisa mjadala huu

(*Applause*)

Kwa sababu hawa watoto wakianza kushikwa kutajulikana wa Tanzania, watajulikana wa Uganda, watajulikana wa Mariakani na wa Mwakirunge.

Kwa hivyo hao kila mmoja ana kwake na wana kwao wataomba kule Mariakani watasaidiwa wa Uganda watakuwa Uganda kwa sababu wale walemavu walikuja wakashikwa wakapatikana wanatoka Tanzania na kuna mtu aliwakodisha waje waombe kisha ikifika jioni wampelekee pesa ilikuwa ni biashara, na mama anafanya kazi anamwambia leta watoto wako nitakushikia kumbe wale watoto aenda nao barabarani aende akaombe akishaomba yule mama jioni ana kitu fulani anapewa na wale watoto wanapewa muda wa kwenda kutafuta pesa ama kiwango cha pesa, haswa watoto wale wanakosa heshima watakuwa hawana malezi mazuri na ukifungua dirisha la gari wanatukana watu.

Kwa hivyo hii ipitishwe ni Mswada mzuri sana na hao wa Mwakirunge wataomba Mwakirunge...

(*Laughter*)

Na wa Uganda wabaki Uganda, Tanzania wabaki Tanzania, na sisi pwani yetu iwe safi na kuwe kuzuri watoto tupate wa maana hao watoto kisha watakuwa wakora waanza hivyo pole pole kisha wanakuwa wakora. Ahsante.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Lucy Chizi.

**Hon. (Ms) Chireri:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, mimi pia naunga mkono hoja hii moja kwa moja...

(*Applause*)

Mheshimiwa Spika mji wetu wajibu wetu, Mombasa Kaunti ni mlango wa nchi wageni wote ni lazima waingie Mombasa Kaunti ndio waende nchi jirani; hizi tabia ambazo ni za kuranda randa zinatuaibisha wanaoingia kuomba omba watoto wanaomba omba kina mama, uzuri wa familia ni familia ikae ambapo itaelewa watapata malezi bora, chakula bora lakini unashangaa wageni tuliowapata lakini wageni ambao ni balaa.

Wageni hawa wanatufanyisha tuwe mafukara katika Mombasa yetu hii, inafanyisha mji Mheshimiwa Spika kuwa mchafu.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika hawa watu wakipatiwa, hizi familia zikipatiwa mahali maalum ambapo watakaa wengine watasema kama wanenaji waliotangulia kusema hawa

wakiwekwa pamoja wengine watasinywa na yale maisha ya hawa watarudi kwao kama ni Mwakirunge, kama ni Tanzania kama ni wapi hawatachafua mji wetu tena...

*(Applause)*

...Ni aibu Mombasa Kaunti kuwa kuna watu wa kuomba omba kama ambaye Gavana wetu hawezi kutulea na sisi tuna nguvu na Gavana wetu yuwaweza kutulea tukawa na maisha bora lakini yale maisha ambayo tunaonyeshwa ni ya kudhalilishwa ni watu ambao wanakuja katika nchi jirani na kutuabisha sisi kama Kaunti ya Mombasa.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika hawa watu watengewe mahali na tutawafukuza na tumesikika wengine wana kura zetu tukiwachukua na tukiwatengea mahali zile kura hazijakimbia ni zetu na watatupigia lakini mji wetu tuusafishe na kuusafisha hizi familia ambazo zinaranda randa ovyo tuzitafutie mahali tuzitenge.

Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Duncan Onyango...

**Hon. Onyango:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nashangazwa na Waheshimiwa wenzangu sijui wameelewa maana ya mada hii maana mada hii wanasema wanaiunga mkono lakini ni kama wanaipinga.

Mheshimiwa Spika mimi msimamo wangu hapa ni kuupinga huu mswada naeleza sababu za kuupinga...

*(Applause)*

...na nikianza na yale yaliyozungumzwa ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa ya kwanza, nimesikia ya kwamba kuna *Bill*, serikali ya Kaunti sijui imetenga pesa ya kuweka vituo vya kuokoa havijawekwa ndio watu wako katika mipangilio ya kuweka vituo hivyo mpaka wa leo havijawekwa.

Mheshimiwa Spika ni vizuri ikiwa kweli serikali ya Kaunti inataka kuwaondoa katika zile sehemu ambazo kwamba ziko ni hizi vituo vya kuokoa zijengwe kwanza; wajua utatoa mtu ilhali haujajipanga hujui utamtoa kumpeleka wapi ni sawa sawa na kwenda kufukuza wachuuzi na hujawatengea soko mahali, unawaambia tokeni hapa kauzeni vitu vyenu hapa haina tofauti.

Mheshimiwa Spika tumesikia na Mheshimiwa mwenzangu anawakilisha wodi ya Likoni ya kwamba alikuwa na wapangaji ina maana yule ni mtu ambaye anajitegemea hataki kutegemea Kaunti na wakati mtu anakwenda kuomba hajaiba akikuomba ni wewe uwe na roho ya imani uingie mwenyewe mfukoni umpe hajakunyanganya.

Kwa hivyo tunapeana kwa hiari Mheshimiwa Spika ikiwa mtu ameamua kujiajiri ameenda ameomba ikifika mwisho wa mwezi anahakikisha amelipa kodi ya nyumba ....

*(Interruption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes, Hon Mary Akinyi...

**Hon. (Ms) Akinyi:** Ningependa tu kufahamisha Jumba hili ya kuwa hawa wanao omba ijapokuwa kuomba si vibaya lakini akikuomba ukimnyima yuwakutusi na ni watoto...

*(Applause)*

...akikuomba tu ukimnyima yuwakutusi na ni mtoto sasa hapo kuomba kuna uzuri gani? Halafu ile *Bill* ambayo ilikua nasema ni *Act* ambayo sasa ni kitu ambayo inaendelea kufanya kazi.

**Hon. Onyango:** Mheshimiwa Spika nafikiri mimi ni mzaliwa wa hapa na kila siku mimi huombwa kama sina, sina na kama ninazo huwa napeana lakini sijawahi kutukanwa, kwa hivyo hio mimi na tofautiana sana na Mheshimiwa anayesema ukiwanyima wanakutukana mimi sijawahi tukanwa.

Mheshimiwa Spika tulifahamishwa ya kwamba kulikuwa na wapangaji na aliyezungumza alikuwa shahidi mzuri sana ya kwamba yule mama alikuwa anahakikisha amemlipa kodi ya nyumba mwisho wa mwezi leo mama yuko na watoto wake na hana kazi, utakuta yule mama ni mjane wale watoto ni mayatima tegemeo la yule mama ni aje aombe

apate shilingi mia watoto wake wakale ama aweke kidogo kidogo ikifika mwisho wa mwezi aweze kulipa kodi.

Leo munasema yule mama mumtoe pale hamjatenga pesa za kusaidia watoto mayatima, Kaunti haijatenga pesa ya kusaidia kina mama wajane sasa hii ni kutengeneza tunatengeneza ama tunaharibu zaidi?

Mheshimiwa anasema ya kwamba wanachafua mji mimi natofautiana nao sana mji kama ni mchafu ni mchafu watolewe wasitolewe kama mji ni mchafu utabaki kuwa mchafu...

*(Applause)*

...Mheshimiwa Spika wale ni binadamu si takataka na zinazochafua mji sote tunaelewa ni takataka juzi tu amekuja na mswada mara taka zibebwe usiku, mara zibebwe mchana....

*(Applause)*

...Kama mji ni mchafu ni mchafu hata mkazoa taka saa nane za usiku bado taka zitakuwepo Mheshimiwa Spika.

Katika katiba yetu wale ni binadamu na wako na haki zao na tusifanye jambo ambalo kesho tutajipata kortini manake mwaweza wadharau wale ni omba omba ukawanyima haki zao Kaunti hii ya Mombasa tukajipata taabani ya kwamba wale omba omba wameshirikiana wamechukua wakili kama James Orengo leo serikali ya Kaunti inakwenda kortini kufanya kesi baina ya wao omba omba na serikali ya Mombasa.

Mheshimiwa Spika mimi ningeomba waheshimiwa wenzangu ya kwamba hizi tunasema ni *Bills* ama tunasema ni sheria na kuna Mheshimiwa amesema ya kwamba kuna pesa zimetengwa katika serikali kuu ya kuweza kuwahudumia hawa watoto kina mama na familia zinazoomba.

Kunacho kitengo husika katika hii serikali ya Kaunti wangeshauriana na serikali kuu wahakikishe ya kwamba zile pesa ziko na ni mikakati gani serikali kuu iko nayo ya kuhakikisha ya kwamba hawa watoto wameondolewa na kina mama maanake hawa naona wanasisitiza watoto pekee yake lakini katika huu mjadala kuna familia za watoto omba omba na kuna wanao omba omba, sasa sijui *beggars* na familia na sijui...

Mheshimiwa Mswada wenyewe unachanganya ukikuja hapa, *NOTING THAT the street families, street children and beggars are mostly children who are between the ages of 10 and 16*, Mswada wenyewe unachanganya ukusoma kwa makini.

Aliokuja na mjadala huu anatuchanganya maanake hata mimi sijaelewa ametuambia nini na waheshimiwa waliozungunza naona wanadai watoto lakini ukija hapa nafikiri hata mwenye hoja hii ukimuuliza vizuri atakuambia yeye mwenyewe hajui...

*(Laughter)*

...maanake ikiwa sote hatuelewi basi hata yeye haelewi. Mimi nakuomba katika heshima na taadhima Mheshimiwa Spika kabla hujafanya uamuzi tuhakikishe ya kwamba wale watoto na mimi nakuhakikishia kwamba wengi wao ni mayatima, wale kina mama wana omba omba pale wengi wao ni kina mama wajane, kabla hatujawatoa tuhakikishe ya kwamba haki zao hatujawanyima tuhakikishe ya kwamba Serikali yetu ya Mombasa iko na mikakati ya kuona kwamba mtu yeyote atakayetolewa pale kwa kuomba kuna mahali pazuri tutawaweka kama ni shule watoto wataenda kina mama tuwafungulie biashara zao na hivi tutakuwa tumefanya jambo la busara. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Kithinzi.

**Hon. (Ms) Zainab Kithinzi:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika Mswada ulioletwa ni Mswada mzuri, ni Mswada mzuri ulioletwa na umeletwa kwa wakati unaofaa kwa sababu kama tunavyoelewa kweli kuna waombaji kule barabarani na kama tunavyoelewa ni binadamu wanakula na wanashiba vizuri na chakula....

*(Interruption)*



**Hon. Onyango:** Mr. Speaker....

*(Interruption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon Duncan Onyango what is it?

**Hon. Onyango:** Mr. Speaker kindly allow me to remind this Honourable House that we don't have quorum. Thank you.

*(Laughter)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Clerk can you ascertain whether there's quorum in the House

*(Clerk confirmed lack of quorum)*

Sergeant at Arms Can you ring the quorum bell?

**Hon. (Ms) Zainab Kithinzi:** Mheshimiwa Spika...

*(Interruption)*

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Kithinzi what is it?

**Hon. (Ms) Zainab Kithinzi:** Mheshimiwa Spika Mheshimiwa anayesema hakuna quorum...

*(Interruption)*

*(Sergeant At Arms rung the quorum bell)*

**Hon. (Ms) Akinyi:** Mr. Speaker?

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes what is it?

**Hon. (Ms) Akinyi:** Please if you don't mind can you allow me to act as a Chief Whip?

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes you can go if there is no Chief Whip or Deputy Chief Whip? Okay then Hon Mary you can go and Whip.

*(Hon (Ms) Akinyi exited the Chambers)*

**Hon. Ibrahim Kondo:** Am representing the Chief Whip Mr. Speaker.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): No we have assigned that duty to Hon Mary Akinyi. Yes what is it Hon Member of Mwakirunge?

**Hon. Mwinga:** Thank you Mr. Speaker may I clarify something before we get the quorum Mr. Speaker?

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): It's not possible there's no quorum, there's no quorum, and there is no House when there's no quorum...

*(Applause)*

*(Silence)*

*(Hon (Ms) Akinyi entered Chambers)*

Yes Hon Mary?

**Hon. (Ms) Akinyi:** Thank you Mr. Speaker Sir, I have done what I have done as per your permission and I know there's quorum now.

**Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Then we wait for another three, two minutes.

*(Silence)*

Clerk can you ascertain that there is quorum?

*(Clerk confirmed lack of quorum)*

Yes Members since there's no quorum this House is adjourned until tomorrow in the afternoon.

The House rose at 3:21pm.